MATUMAINI PROG NO:2384

TITLE: THE MIND DETERMINES THE WAY A PERSON LIVES

SUMMERY: KINAANGAZIA KUHUSU VILE AMBAVYO AKILI HUTUNENEA KWA KUAFIKIA MAAMUZI YETU YA KUISHI.

TEXT: WAEFESO 4:17-24

MADA: AKILI NDIYO HUTUAMULIA MANMA TUNAVYOISHI

……

U hali gani rafiki yangu popote ulipo huku nikiwa nanyenyekea tena mbele zako ili kukushukuru kwa kuunganika pamoja nami tena kupitia kwa upendo Wake Mwenyezi Mungu na lengo la kufunzana kuhusu Neno Lake Mwenyezi Mungu.

Nakukaribisha katika kipindi hiki cha Matumaini kutoka TWR Nairobi.

Natumai ya kwamba, tangu wakati wa Mwisho kupatana nawe, ungali mzima katika Bwana.

Leo hii pia tunaendelea na mafundisho yetu kutoka kwenye Waraka huu wa mtume Paulo kwa Waefeso sura yake ya nne kuanzia aya yake ya kumi na saba hadi ile ya ishirini na nne (Waefeso 4:17-24)

Katika waraka huu, mtume Paulo anazungumzia kuhusu vile ambavyo akili ya kila mmoja wetu huumualia jinsi aishivyo.

Kwa kumalizia kipindi cha leo,,,mpendwa,,nitakuwa nashiriki nawe anwani yangu kwa sababu ya mawasiliano kati yetu.

Jina langu ni Vincent Amara mwanzo nawakaribisha watumishi hawa ambao wanatuambia ukweli kabisa ya kwamba Yesu ndiye njia. Wimbo ukiwa ni Amani nao wana-Ambassadors of Christ .

WIMBO: .....

Ni wana-Ambassadors of Christ na wimbo Amani……

OMBI.Mfalme wa Ajabu tena Baba yetu wa Mbinguni.Tunasema ni asante kwa sababu ya somo hili la leo.Tusaidie katika kulielewa vyema katika jina la Mwanao Yesu Kristo…----Amen

Karibu tena katika kipindi hiki cha Matumaini kutoka TWR ambapo leo hii tunajifunza kuhusu **vile ambavyo akili humuamulia mtu namna ya kuishi** huku ujumbe wetu tukiutoa kwenye Waraka wa Mtume Paulo kwa Waefeso 4:17-24.

Mpendwa,, “kama vile mtu awazavyo moyoni mwake,,,hivyo ndivyo alivyo” Hayo sio maneno yangu hata kidogo rafiki yangu.

Haya ni maneno ambayo Bwana wetu Yesu Kristo alikuwa akimnukuu mtu mwenye hekima zaidi aliyepata kuishi.

Ningependa ukalitafakari kulihusu hilo maana katika akili zetu sisi huamua jinsi tunavyoishi.

Mtu anapowazia mabaya,,,bila shaka mtu huyo ataingia katika kuyatenda mambo ambayo ni maovu.

Naye yule mtu,,anayeyawazia mema,,,atayafanya yaliyo mazuri.

Rafiki yangu,,,katika akili hizi zetu,,sisi tunauhitaji msaada zaidi katika kuyawaza yaliyo mema na zaidi sana yanayofaa.

Msaada wetu hebu nikuhakikishie ya kwamba,, unatoka kwake Mwenyezi Mungu na Neno lake.

Hii bila shaka ndiyo sababu ambayo ninataka nikushirikishe kutoka kwenye waraka huu wa Mtume Paulo kwa Waefeso 4:17-24. Kuhusiana na waraku huu nataka tuone kile Mtume Paulo alikisema kuhusu vile akili ya mtu humuamulia jinsi anavyoyaishi maisha yake.

Nasoma;

17. Basi nasema haya, tena nashuhudia katika Bwana, kwamba tangu sasa msienende kama waenendavyo Mataifa wengine, katika ubatili wa nia zao;

18. akili zao zimetiwa giza, nao wametengwa na uzima wa Mungu kwa sababu ya ujinga uliomo ndani yao, kwa sababu ya upofu wa mioyo yao;

19. ambao wamezimia, wamejitia katika ufisadi na kufanya uchafu wote kwa kutamani.

20. Lakini ninyi hamkumjifunza Kristo hivyo;

21. ikiwa mmemsikia na kufundishwa naye, kama kweli ilivyo katika Yesu;

22. Vueni kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa kale, unaoharibika kwa kuzifuata tamaa danganyifu;

23. Mfanywe wapya katika roho ya nia zenu;

24. Vaeni utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli.

Dadangu,,ili kuelewa jinsi ambavyo akili hutuamulia namna ya kuishi,,Mtume Paulo anayaelezea ***Masharti*** Kadhaa ya vile akili zetu huyaathiri maisha yetu.

Sharti la kwanza kabisa ambalo mtume anatuelezea ili kutuonyesha vile tulivyoanza ni kuhusiana na hali ya akili isiyokuwa na maaarifa

Hapa tunamwwona mtume huyu akiandika kuhusina na mienendo ya watu wa mataifa mengine.

Alisema wanatembea katika ubatili wa akili zao, utupu, ufinyu wa akili zao.

Tunapoangazia vizuri zaidi,,tuaona ya kwamba alikuwa akielezea kuyahusu mawazo ya watu ambao hawajaokoka.

Sasa nataka uone kwamba akili hii bila ya maarifa ni giza. Aya ya 18, inaelezea ya kwamba,,,kuwa na ufahamu umetiwa giza na kutengwa na uzima wa Mungu.

Hii ina maana ya kwamba,,akili ya asiyeamini inatiwa giza,,,inaendelea na kusema “kupitia ujinga uliomo ndani yake.” Yaani mtu kama huyo,, hawaelewi na hata zaidi sana hatambui kile anachokifanya hata kidogo.

Kama tulivyo tangulia kusema ni kwamba,,,akili ya ujinga huwaongoza watu katika njia ya kupotea mbali na Mungu.

Sharti la pili ambalo Mtume Paulo anaelezea ni …kuhusiana na hali ya akili yenye maarifa.

Mtume Paulo anatuambia katika mstari wa 20 kwamba “hatukujifunza Kristo hivyo.” Kwa maneno mengine tunazo habari ambazo wale watu ambao ni makafiri hawana.

Rafiki yangu,,kwa roho ya ndani,,kuwa tu na ufahamu ya kwamba,,,unaposikia kuuhusu ukweli uliopo katika Kristo,,,mara moja akili hufungukuka kumhusu.

Katika mstari wa 21,,Mtume Paulo aliandika na kusema “na tumefundishwa naye, kama kweli ilivyo ndani ya Yesu.”

Sasa rafiki, njia pekee ya kupata ukweli ni kumjua Yesu katika mawazo yako, moyoni mwako na zaidi sana katika uzoefu wako kibinafsi.

Akili yenye maarifa,,hutuondolea maisha ya zamani mpendwa na kutufanya upya.

Jambo la tatu na mwisho ambalo hutufanya upya katika Kristo,, ni kufuatia ***hali ya akili iliyofanywa upya ndani mwetu.***

Mtume Paulo kwa hakika anatoa amri hii: “Na mfanywe wapya katika roho ya nia zenu.”

Mpendwa katika kuliafikia hili,,,ni lazima mtu kuwa mnyenyekevu kabisa.

Anaendelea kutufundisha katika mstari wa 24 kwamba hatupaswi kuahirisha tu, kama alivyotaja katika mstari wa 22, bali pia kuvaa.Yaani kuuvaa utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli.”

Hiyo ina maana kuwa na roho mpya tu,,,ndiye hutuongoza katika haki na utakatifu wa kweli, kwa msaada wa Mungu.

Ndugu ,,,kutokana na somo la leo,,tumeweza kuona ya kuwa ni akili zetu ndizo hutuamulia namna ya kuishi na zaidi sana kuyadhibiti yale yote ambayo sisi hufanya.

Kwa hivyo mpendwa,,sisi kama wana wa Mungu tunapaswa kuomba kwa ajili ya kufanywa upya. Hii ikiwa ni kufuatia hamu yetu ya ndani kabisa.

OMBI.. Mfalme wa Waflme Uliye tukuka kuliko kila kiwaaacho chote.,, ,,tunakushukuru kwa somo hili la leo kuhusu vile akili zetu hutuamulia maisha yetu. Tunakuomba ukatuongoze zaidi katika kuzitumia hizi akili zetu ili kukutumikia vyema,,,Nawe kwa imani tunajua ya kwamba utatuongoza katika jina la Bwana wetu Yesu Kristo…..Amen.....

Kimekuwa ni kipindi chako cha kujifunza neno Lake Mwenyezi Mungu.Kipindi cha matumaini kutoka Twr ambapo siku hii ya leo tumejifunza vile akili zetu hutuamulia namna tunavyoishi.

Ujumbe wetu tumeutoa kwenye kitabu cha Waefeso 4:17-24.
Kama umeweza kubarikiwa,au ana kitu ambacho ungependwa kusema nasi au hata maswali ya Bibilia, tafadhali zungumza nasi kupitia kwa anwani nitakayoshiriki nawe baada ya wimbo huu ambao unasema ya kwamba,,,Nimeamua kumfuata Yesu,...naye ndugu yetu Vaisi Charles

WIMBO…….

Ni kweli kabisaa,,ukiamua Vyema katika kumfuata Yesu Kristo,,,utakuwa umeamua vyema. Akiwa ni ndugu yetu Vaisi Charles na wimbo Nimeamua kumfuata Yesu.....

ANDIKA BARUA AU UJUMBE WAKO UKIANZA NA NENO MATUMAINI TWR NA KUTUMA KWA:
SLP 21514 CODE 00505
NAIROBI KENYA x2
Simu/Sms 0721970520 x2
Barua Pepe-barua@twr.co.ke